GREDI YA I

MTIHANI WA MWISHO WA

MUHULA WA KWANZA 2023

KISWAHILI SEHEMU YA A

1. Kusikiliza na Kuzungumza
2. Kusoma kwa sauti

Jina_________________________________________

Shule_________________________________________

Gredi_________________________________________

Jinsia

Mvulana_________ Msichana___________

<u>KWA MATUMIZI YA MTAHINI</u>

Tumia vigezo na viwango vya kuthaminia vilivyopewa kwenye mwongozo wa mwalimu.

| ZOEZI | | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1. | Kusikiliza na kuzungumza | |
| 2. | Kusoma kwa sauti | |

## ZOEZI LA KWANZA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

SEHEMU YA KWANZA

- Jitambuslishe kwa kusema "Mimi ni mwalimu....."
- Muuliza mwanafunzi jina lake

  ______________________________

a) Taja umri wako. (mwanafunzi ajibu)
b) Je, wewe ni msichana au mvulana? (mwanafunzi ajibu)

SEHEMU YA PILI

i) Msomee mwanafunzi kifungi kifuatacho mara mbili.
ii) Mjulishe mwanafunzi kuwa atajibu maswali baada ya kusoma.

Nilipoamka asubuhi nilimpata baba ameketi sebuleni akinywa chai. Nilimuamkua, "Shikamoo baba", naye alinijibu, "Marahaba mwanangu," Baba alifurahi kuona nilijua kuamkua wakubwa wangu. (Mwalimu arudie)

a) Nilipoamka nilimpata nani?
b) Jibu la shikamoo ni nini?
c) Kwa nini baba alifurahi?

ZOEZI LA KUSOMA KWA SAUTI

Ukiwa tayari kuanza tathmini sema;

"Sasa naomba unisomee kifungu hiki kwa sauti."

Ni vyema watoto kuwa na heshima kwa wakubwa wao. Iwapo mtoto amamkosea mwenzake amwambie pole. Akipewa kitu aseme asante. Pia mtoto anapotaka kitu ama kuomba ruhusa atumie maneno "tafadhali" ama "nisaidie".

Pia ni vizuri kuomba msamaha unapokosea mwenzako.

(maneno 40 kwa dakika 1)